


Pata anwani ya barua pepe

Barua pepe ni nini?

Barua pepe ni anwani ya barua ya kielektroniki unayoweza kutumia kuwasiliana na watu wengine.

Aghalabu unahitaji anwani ya barua pepe ili kutumia huduma za mtandaoni za shule, kazini, benki, famasia, ofisi za daktari, na sehemu nyinginezo.

Unaweza kupata anwani ya barua pepe bila malipo. Kuna sehemu tatu za anwani ya barua pepe:



Ni muhimu kukumbuka anwani yako ya barua pepe na nywila. Chagua jina la mtumiaji ambalo ni rahisi kukumbuka na ni sehemu ya jina lako. Chagua nywila ambayo ni ngumu kwa wengine kukisia.

Nawezaje kupata anwani ya barua pepe?

1. Chagua mtoa huduma za barua pepe:

- Gmail.com (inapatikana kwa lugha 70 tofauti)
- Outlook.com

2. Tumia nambari yako ya simu kuthibitisha akaunti yako

3. Jaza fomu Ingiza:

- jina la kwanza
- jina la mwisho
- jina la mtumiaji unalotaka kutumia
- nywila thabiti ambayo utatumia tu kwa akaunti yako ya barua pepe
- nchi
- tarehe ya kuzaliwa

4. Ingiza nambari yako ya simu

5. Thibitisha akaunti yako. Ingiza nambari ya kuthibitisha uliyotumiwa kwenye simu yako.

6. Kubali sera ya faragha

Tazama video ili kupata maelezo zaidi kuhusu kujiandikisha kutumia barua pepe na kuitumia salama:

Kiingereza - <https://www.digitallearn.org/courses/intro-to-email-new>

Kiingereza - <https://www.digitallearn.org/courses/intro-to-email-2-beyond-the-basics-new>

Kiingereza - <https://www.digitallearn.org/courses/online-fraud-and-scams-new>

Kiingereza - <https://edu.gcfglobal.org/en/topics/emailbasics/>

Kihispania – <https://www.digitallearn.org/courses/introduccion-al-correo-electronico-nuevo>

Kihispania – <https://www.digitallearn.org/courses/introduccion-al-correo-electronico-2-nuevo>

Kihispania – <https://www.digitallearn.org/courses/fraude-y-estafas-en-linea-nuevo>

Kihispania – <https://edu.gcfglobal.org/es/crear-un-correo-electronico/>